



LOWELL PUBLIC SCHOOLS
Ofisi za Usimamizi wa Kati Henry J. Mroz
155 Merrimack Street
Lowell, MA 01852

Februari 5, 2021

Wapenzi Wanafunzi, Familia na Wafanyikazi wa Lowell Public Schools,

Ninatarajia kwamba barua hii itakupata ukiwa mwente usalama na afya. Nina furaha kuripoti kuwa mienendo ya mwisho kabisa katika data ya COVID-19 hapa Lowell yanadokezea kwamba tunaweza kutimiza lengo letu la kurejesha kundi letu la kwanza la wanafunzi kwa mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi shuleni baada ya likizo la Februari.

Kwa hivyo, tunawapangia wanafunzi wetu katika programu za elimu maalum iliyo tofauti zaidi na mafunzo ya kawaida – ambao walikuwa wanashiriki katika mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi hapo awali – warejelee shuleni kuanzi Jumatatu, Februari 22.

Vivyo hivyo, bado pia tunafuata mpango wetu wa awali wa kuwarejesha kundi letu la pili la wanafunzi siku ya Jumatatu, Machi 1 – wanafunzi hao, ambao ni wale wasio katika programu za elimu maalum zilizo tofauti zaidi na masomo ya kawaida, lakini waliohudumiwa kibinafsi mwaka huu wa shule kama mpango wetu wa awali wa kufungua shule upya .

Kila Alhamisi, Jimbo huru hutoa muhtasari wake wa COVID-19 uliyo na msingi wa jamii. Ripoti ya wiki hii inaonyesha kwamba viwango vya COVID-19 hapa Lowell zinaendelea kuboreka. Kiwango cha maradhi ya kila siku katika wakaazi 100,000 kwa sasa ni 63.2, ambayo imeshuka kutoka 72.5 wiki iliyopita, 87.0 wiki mbili zilizopita, na chini zaidi ya 134.4 ambayo ilikuwa kiwango cha maradhi ya kila siku katikati ya Disemba. Wakati huo huo “kiwango cha asilimia ya watu wanaopatikana na maradhi” (asilimia ya uchunguzi zinazopatikana na maradhi hapa Lowell) kwa sasa ni 7.10, ambayo ni chini ya 8.37 ya wiki iliyopita, 10.15 ya wiki mbili zilizopita, na chini zaidi ya 12.33 ambayo ilikuwa kati ya Disemba.

Familia ya wanafunzi inayopangiwa kurudi kwa mafunzo ya kuhudhuria Februari 22 au Machi 1 watapokea taarifa zaidi kutoka shule zai. Tutawasiliana pia wiki ijayo na mawasiliano ya wilaya inayotoa taarifa zaidi kuhusu usafirishaji, usalama wa COVID-19, na matumizi ya uchunguzi wa kikundi unaogharamiwa na jimbo wa COVID-19.

Wakati huo huo, iwapo mtoto wako HAKUhudhuria shule wakati wowote katika mwaka huu wa shule, tafadhali tumia madakika machache na [ujaze utafiti huu](#) unaopima hamu yako, iwapo unayo, kwa mtoto wako kuweza kushiriki katika mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi baadaye mwaka huu wa shule. Aprili 1 utabaki kuwa tarehe letu tunaolenga kupanua mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi kwa wanafunzi zaidi ya wale walioteuliwa kuhudhuria hapo awali katika mwanzo wa mwaka shule huu.

Tunaendelea kuwa wenye shukrani kwa ushiriki wako na uwezo wako wa kubadilika kirahisi katika mgogoro huu wa kiafya usiyoonekana hapo awali na tunatarajia kuwakaribisha wanafunzi wetu tena shuleni katika siku zijazo za karibu.

Wako Mwaminifu,

Dr. Joel D. Boyd
Mkuu wa Mashule